

# Alien Emergency Medical (AEM)

## Uchunguzi na matibabu ya COVID-19

### Usuli

Alien Emergency Medical (AEM) ni mpango kwa ajili ya watu wanaokidhi vigezo vya matibabu ya dharura lakini hawakidhi vigezo vya utaiifa au uhamiaji, au mtu anayekidhi vigezo ambaye hajatimiza miaka 5 ya sheria.

Dharura zinazostahiki zinajumuisha:

- Ziara za chumba cha dharura
- Ukaaji hospitali kwa wagonjwa waliolazwa
- Upasuaji wa wagonjwa wasio wa kulazwa
- Dialisisi
- Matibabu ya saratani
- Matibabu ya mgonjwa aliyepandikizwa viungo vya mwili

### Taarifa ya mpango

Kutokana na [janga la COVID-19](#) Mamlaka ya Huduma ya Afya (HCA) imewasilisha [sheria ya dharura](#). Sheria hii inaongeza:

- Dharura zinazostahiki kujumuisha uchunguzi na matibabu ya COVID-19.
- Mazingira ya vipimo na matibabu yanajumuisha ofisi, kliniki, au huduma za afya kutoka mbali.
- Huduma zilizoidhinishwa. Watu waliogundulika kuwa na maambukizi ya COVID-19 wanaweza kupatiwa dawa na huduma za upumuaji. Watu waliogundulika kuwa na maambukizi ya COVID-19 wanaweza kugharamiwa ziara za ufuatiliaji na dawa.

### Jinsi ya kutuma maombi

Watu wazima wenye umri wa miaka 19 hadi 64:

- **Mtandaoni:** tembelea [Washington Healthplanfinder](#)
- **Programu ya Simu:** Pakua [programu ya WAPlanfinder](#)
- **Karatasi:** [Maombi ya Kugharamiwa Huduma ya Afya \(18-001P\)](#)
- **Simu:** 1-855-923-4633

Watu wazima wenye miaka 65 au wazee zaidi, kipofu, mlemavu, au mwenye mahitaji ya huduma za muda mrefu:

- **Mtandaoni:** [Washington Connection](#)
- **Karatasi:** [Maombi kwa ajili ya kugharamiwa huduma ya uzee, upofu, ulemavu/matibabu ya muda mrefu \(18-005\)](#)
- **Simu:** 1-877-501-2233

Laha ya juu ya faksi ya AEM inajumuisha COVID-19 chini ya sehemu ya Kuomba Kugharamiwa Huduma.